LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

# Mlinzi wa HAKI

Toleo la Kiswahili

Ishu Na. 02 Januari - Machi 2018



## Yaliyomo


04 Wabunge Wanawake waunga Mkono Kampeni Kupinga Ndoa za Utotoni

10 Wadau: Katiba Mpya Itadumisha Demokrasia na Amani nchini

12 LHRC yawalilia Akwilina, Luena yataka Uwajibikaji


# Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake

Katika kusheherekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake ambayo huadhimishwa Machi 8 kila mwaka tangu siku hiyo ilivyoidhinishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1975, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeungana na marafiki wa haki kote ulimwenguni kuadhimisha siku hiyo nchini Tanzania.

.......*Inaendelea Uk. 11*

# Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji

Salaam ndugu msomaji, Karibu katika toleo rasmi la jarida letu la Mlinzi wa Haki, jarida hili ni la pili tangu kusajiliwa rasmi na kupata leseni ya uchapishaji wa jarida letu. Mlinzi wa Haki ni jarida linalobeba dhana nzima ya kazi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambayo ni utetezi na ulinzi wa haki za binadamu. Toleo hili linajumuisha taarifa ya kazi zilizofanyika katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tumeuanza mwaka 2018 tukiwa na ari mpya ya kuendeleza utetezi wa haki za binadamu kwa lengo la kuifikia jamii yenye haki na usawa.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi Kituo kimefanya shughuli mbalimbali ambazo zina mchango mkubwa katika kuimarisha hali ya haki ya haki za binadamu na utawaa wa sheria nchini. Moja ya matukio makubwa ni pamoja na maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake ambapo Kituo kiliwakutanisha wanawake kutoka katika kada mbalimbali kusheherekea mafanikio ya wanawake sambamba na kuimarisha mikakati ya namna ya kuboresha ustawi wa haki za wanawake nchini Tanzania. Pia Kituo kiliitisha mdahalo wa uliowakutanisha wadau kutoka sekta kujadili mchango wa katiba katika kuimarisha demokrasia na amani nchini. Kituo pia kimeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika maendeo tofauti ya nchi ikiewemo Mradi wa Kutokomeza Ukeketaji huko wilayani Serengeti Mara; Mradi wa Kuwezesha Wasichana na Wanawake Wadogo ili Kuiwajibisha Jamii kutoa Huduma bora za Afya ya VVU/UKIMWI mkoani Shinyanga; Mradi wa Kuzuia Ufurutu Aga mkoani Arusha na Tanga; Mradi wa Uwezeshaji wa Kisheria Mijini jijini Dar es Salaam pamoja na Mradi wa Kupanua Ushiriki wa Wananchi.

Kituo kimeendelea na shughuli mbalimbali za uchechemuzi ikiwemo utoaji elimu kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, kwa ujasiri mkubwa Kituo kimeendelea kukemea vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria kwa kuzikumbusha mamlaka na wananchi kufuata sheria na kuheshimu haki za binadamu. Katika kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka Kituo kimetoa matamko kukemea ukiukwaji wa haki ya kuishi uliotokea katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo mauaji ya kikatili yaliyotoea kwa Godfrey Luena na mwanafunzi Akwilina Akwilini. Kupitia matamko hayo Kituo kimezitaka mamlaka pamoja na wananchi kwa ujumla kuwajibika katika kulinda haki za binadamu.
Vile vile Kituo kimeendelea kutoa msaada wa kisheria kwa watanzania wasio na uwezo wa kufikia gharama za haki. Kupitia Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Kinondoni pamoja na Kituo cha Msaada wa Kisheria Arusha na pia kupitia huduma za msaada wa kisheria wa kuhama hama LHRC imewasaidia jumla ya watanzania 2,577 (849 Wanawake na1728 Wanaume) kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2018. Zaidi ya hapo, Kituo kimefungua vituo vinne (4) vipya vya msaada wa kisheria katika kata nne tofauti ambazo ni Somangila na Kibada katika wilaya ya Kigamboni pamoja na Mnyamani na Kitunda katika wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam.
Kituo kimefanya mengi kana kwamba ni ngumu kuyaweka kwa ufupi katika ukurasa mmoja. Furahia kulisoma jarida letu kwa undani ili uweze kufahamu zaidi kuhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na kazi zake. Usisite kutoa maoni kwa kadiri utakavyoona inafaa.
Wakatabahu,



**Dkt. Helen Kijo Bisimba**
**Mkurugenzi Mtendaji.**

# Tahariri

Habari Rafiki wa Haki,
Karibu katika jarida letu la Mlinzi wa Haki, jarida hili linajumuisha taarifa za kazi zilizotekelezwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa kipindi cha Januari mpaka Machi, 2018. Katika kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka 2018 Kituo kimeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za utetezi wa haki za binadamu kwa nia ya kufikia maono ya Kituo ambayo ni kufikia Jamii yenye Haki na Usawa.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka Kituo kimefanya matukio kadhaa ya kukumbukwa ikiwemo maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake pamoja na mdahalo wa wadau kujadili mchango wa katiba katika kuimarisha demokrasia na amani nchini. Hata hivyo LHRC imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali yenye lengo la kuwawezesha watanzania kupata uelewa wa haki za binadamu na kuweza kuwajibika kulinda haki za binadamu na utawala wa sheria. Vilevile LHRC imeendelea na utetezi na utetezi wa haki za binadamu kwa kutoa matamko kadhaa kukemea ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwemo tamko kukemea kuuawa kwa mwanafunzi Akwilina Akwili pamoja na kuuawa kwa mwangalizi wa haki za binadamu Godfrey Luena.

Hata hivyo Kituo kimeendelea na utoaji wa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Huduma ya msaada wa kisheria na uwakilishi wa wateja mahakamani imeendelea kupitia vituo vyetu vya msaada wa kisheria Kinodnoni na Arusha na hata kupitia huduma za msaada wa ksheria za kuhama hama ambapo jumla ya wananchi 2,577 (849 Wanawake na1728 Wanaume) wamefikia kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2018.



Karibu jisomee zaidi jarida la Mlinzi wa Haki kufahamu mengi zaidi kuhusu kazi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.
Wasalaam,

**Michael Mallya**
**Afisa Mawasiliano**

# Wabunge Wanawake waunga Mkono Kampeni Kupinga Ndoa za Utotoni

Kufuatia mkutano uliondaliwa na mashirika 49 chini ya Mtandao wa Kupinga Ndoa za Utotoni Tanzania (TECMN) ukiwakutanisha wabunge wanawake wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wawakilishi wa mtandao huo kutafuta suluhu ya namna ya kutokomeza ndoa za utotoni nchini; Wabunge Wanawake wameonesha wazi kufurahishwa na kampeni hiyo na kuahidi kuungana na TECMN kushiriki kampeni ya kutokomeza ndoa za utotoni.

Katika mkutano huo ambao Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilishiriki kama mwanachama wa Mtandao wa TECMN, pia walifanikisha kukutana na wajumbe ya Kamati ya Katiba na



*Timu ya Mtandao wa TECMN katika picha ya pamoja na Kamati ya Bunge ya huduma za kijamii*




*Timu ya Mtandao wa TECMN katika picha ya pamoja na Wabunge Wanawake*

Sheria sambamba na Kamati ya Huduma za Kijamii ambapo wote walikubaliana na lengo la kampeni hiyo ambayo ni kubadilisha kipengele cha umri katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kutoka umri wa msichana kuolewa kuwa miaka 15 hadi miaka 18 sawa na watoto wa kiume.

Sambamba na hilo, Kituo kupitia mtandao wa TECMN kituo kilishiriki mkutano na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika Machi 2, 2018 katika ofisi ya Naibu Spika jijini Dar es Salaam kwa lengo la kufanya utetezi kutokomeza ndoa za utotoni.

Pia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshiriki mikutano kadhaa kwa lengo la kushirikiana na wadau wengaine kutoka ndani na nje ya nchi katika kupinga ndoa za utotoni. Kituo kupitia mtandao wa TECMN kimeshiriki mikutano iliyofanyika Uganda na Kenya kwa lengo la kuimarisha utetezi wa haki za wasichana kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

# Watoa huduma za haki, wasichana na wanawake wadogo wajengewa uwezo kisheria

Katika kuimarisha ubora na ufikiwaji wa haki ya afya nchini Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuwajengea uwezo wanufaika wa Mradi wa Dreams Innovation Challenge ikijumuisha watoa huduma za haki, wataalamu wa afya, maafisa ustawi wa Jamii pamoja na wasichana na wanawake wadogo ili kuwezesha kundi la wasichana na wanawake wadogo kuweza kuiwajibisha jamii kuboresha huduma za afya ya UKIMWI mkoani Shinyanga.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2018, Kituo kimeendesha mafunzo juu ya masuala ya Ukatili wa Kijinsi na jinsi unavyoweza kupelekea maambukizi ya VVU, muundo wa kisheria unavyoathiri utaoji wa huduma za afya ya UKIMWI sambamba na jinsi ya kuzuia maambukizi mapya ya VVU kwa wasichana na Wanawake wadogo.

Wakati wa mafunzo katika Manispaa ya Shinyanga, Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa ya Shinyanga aliwakumbusha washiriki kuhusu hali ya maambukizi mkoani Shinyanga Dkt. Peter Malale aliweka bayana kuwa kwa mujibu wa ripoti mbalimbali ikiwemo ripoti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Shinyanga ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa maambukizi ya VVU na Ukatili wa Kijinsia nchini ikiwa inashika nafasi ya sita kwa maambukizi ya VVU na nafasi ya kwanza kwa Ukatili wa Kijinsia. Dkt. Malale alitaja idadi ya watu wanaoishi na maambukizi ya VVU katika Manispaa ya Shinyanga kuwa 23,060 na kutanabaisha sababu za juhudi za kuzuia maambukizi mapya kulega kuwa ni pamoja na




*Washiriki wa Mafunzo kwa Watoa Huduma za Kisheria wakifanya mawasilisho baada ya majadiliano.*



*Watoa huduma za haki wa Manispaa ya Shinyanga wakiwa katika picha ya pamoja na wawakilishi wa LHRC na IDLO baada ya mafunzo.*

kukosekana kwa kampeni za kutosha juu ya elimu ya afya ya UKIMWI, watu kutokuwa tayari kupima VVU na kuhudhuria huduma za afya, kukosekana kwa vituo vya kutosha vya vinavyotoa huduma ya afya ya UKIMWI sambamba na mila na desturi potofu juu ya VVU/UKIMWI.

Kwa upande wake Bi. Getrude Dyabene ambaye ni mratibu wa mradi huo aliwasihi watoa huduma za haki ambao wanajumuisha mahakimu, polisi, waendesha mashitaka, maafisa magereza na mawakili wa Serikali kuzingatia changamoto zilizopo katika sera na sheria katika kufanya maamuzi ya haki ili kukwepa kuwanyima haki wasichana na Wanawake wadogo.

Katika kipindi hicho pia, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kiliendesha mafunzo kwa wanufaika wa awali wa mradi wa Dreams Innovation Challenge ambao ni Wasichana na Wanawake Wadogo. Machi 19 hadi 23, 2018 jumla ya wasichana na Wanawake wadogo 90 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri ya Mji wa Kahama walijengewa uwezo juu ya haki za binadamu, Ukatili wa Kijinsia na Muundo wa Kisheria na jinsi unavyoathiri huduma za afya ya UKIMWI.
LHRC inatekeleza Mradi Dreams Innovation Challenge katika Halmashauri ya Mji wa Kahama na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga



*Wasichana na Wanawake Wadogo wakiwa katika majadiliano ya vikundi wakati wa mafunzo kuhusu Haki za Binadamu, Ukatili wa Kijinsia na UKIMWI katika Manispaa ya Shinyanga.*

# Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake

*.............Inaendelea kutoka Uk.1*

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimefanya shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa msaada wa kisheria wa kuhama hama kwa lengo la kuwafikia Wanawake katika jumla ya kata nane ambazo ni Kaloleni, Elerai, Themi, Sakina and Olemoti jijini Arusha pamoja na Somangila na Kibada, wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Sambamba na huduma ya msaada wa kisheria Kituo kiliandaa warsha iliyowakutanisha Wanawake wanaharakati Kujadili mustakabali wa haki za Wanawake na kupanga namna ya kuboresha harakati kwa lengo la kuimarisha ustawi wa haki za binadamu na Wanawake. Katika warsha hiyo ambayo ilifanyika Machi 9 nyumbani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Mbezi, Dar es Salaam jumla ya Wanawake 35



*Dkt. Helen Kijo-Bisimba akifurahia jambo na wanawake wengine wakati wakati wa hafla ya wanawake kusheherekea Siku ya Wanawake.*



*Wanawake wakijadiliana wakati ya hafla ya wanawake kusheherekea Siku ya Wanawake*

kutoka maeneo tofauti walihudhuria. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaungana na Jamii ya ulimwengu kutambua Mchango wa Wanawake katika kuchochea maendeleo ya Kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kituo kinawasihi watanzania kuheshimu haki za Wanawake na haki za binadamu kwa ujumla kwa lengo la kufikia malengo endelevu ya dunia ya kufikia Usawa wa Kijinsia ifikapo 2030.

# **Wadau:** Katiba Mpya Itadumisha Demokrasia na Amani nchini

Katika kufikia lengo namba moja la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambalo ni kupata Katiba ya Wananchi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeendelea kushirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo na kupata maafikiano ya pamoja ya namna ya kupata Katiba ya Wananchi. Kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2018, Kituo kimewakutanisha jumla ya wadau 571 ikijumuisha wanasiasa, wanafunzi wa vyuo vikuu, wanahabari, Viongozi wa dini, wanasheria, wasaidizi wa kisheria pamoja na wananchi kwa ujumla Kujadili mchakato wa Katiba Mpya.

Februari 2, 2018 Kituo kiliandaa mdahalo uliofanyika jijini Dar es Salaam kuwakutanisha wadau mbalimbali 61 ikiwemo wanazuoni, wanasiasa, wanahabari, wanafunzi wa vyuo vikuu, wanasheria na wananchi kwa ujumla Kujadili hatma ya mchakato wa Katiba mpya nchini. Katika mdahalo huo uliobeba dhana ya “Katiba na Amani katika Chaguzi” wadau walionesha kuwepo kwa ombwe la Katiba nchini na kwa pamoja kuitaka




*Naibu Katibu Mkuu wa TEC, Dkt. Daniel Dule akizungumza wakati wa mdahalo wa Katiba Mpya.*

Serikali kufufua mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya. Akichangia mada katika mdahalo huo, mwakilishi wa Umoja wa Maaskofu Tanzania Dkt. Daniel Dule alikipongeza Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa kuandaa kongamano ambalo linawaleta watanzania pamoja Kujadili mustakabali wa mambo yanayowahusu. Dkt. Dule alitambua umuhimu wa makongamano kama hayo kwa kile alichokiita kuwa midahalo ni jukwaa kwa wananchi Kujadili masuala yanayowahusu na kutatua changamoto zao kwa njia ya Amani.

Kwa upande wake Wakili John Seka alipendekeza kupitiwa kwa sheria zote zinazosimamia uchaguzi kwa lengo la kuepuka utata unaosababishwa na sheria wakati wa uchaguzi.

Mwakilishi wa wa TCD Prof. Mwesiga Baregu alisema kuwa nchi ina ombwe la Katiba kwani Katiba iliyopo ilishatangazwa kuwa haifai na hatimaye mchakato wa kupata Katiba Mpya ukaanza bila mafanikio. Profesa Baregu aliisihi Serikali kuhuisha na kukamilisha mchakato wa Katiba mpya kabla ya uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu 2020.

Sambamba na mdahalo huo Kituo pia kilifanya mdahalo uliowakutanisha wanafunzi ambao ni wananchama wa vilabu vya haki za binadamu katika Chuo Kikuu cha Mzumbe (Morogoro), Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha St. John. Katika mdahalo huo uliofanyika Morogoro Februari 11, 2018 na kuhudhuriwa na jumla ya wanafunzi 412. Washiriki walionesha shauku ya kupata Katiba mpya.




*Wadau kutoka sekta mbalimbali wakifuatilia mdahalo juu ya Katiba Mpya*

# LHRC yawalilia Akwilina, Luena, yataka uwajibikaji

Mnamo Februai 2018 Tanzania ilishuhudia mauji ya kikatili ya watanzania wawili katika nyakati tofauti. Februari 16, 2018 msichana Akwilina Akwilini ambaye alikuwa mwanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji alipigwa risasi akiwa katika daladala Kufuatia Jeshi la polisi kufyatua risasi kwa lengo la kuwasambaratisha waandamanaji wa Chama Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokuwa wakiandamana kuelekea ofisi za Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kinondoni kutaka mawakala wake kupatiwa vibali kwa ajili ya uangalizi wa uchaguzi. Kwa mujibu wa ripoti mwakala wa CHADEMA walinyinma vibali vya uwakala hadi kuifikia siku moja kabla ya uchaguzi wa Mbunge jimbo la Kinondoni.

Katika kuendeleza harakati za utetezi wa haki ya kuishi, LHRC ilikemea kwa nguvu kitendo hicho na kuitaka Serikali kuziwajibisha mamlaka husika kwa kutumia nguvu kupita kiasi iliyopelekea kupotea kwa maisha ya Akwilini. Hata hivyo Kituo kiliungana na watanzania wote kutoa pole kwa familia ya Akwilina na kushiriki maziko yake.

Sambamba na tukio la Akwilina, LHRC ilipata pigo la kuondokewa na mwanachama wake ambaye pia alikuwa diwani wa Ifakara wilayani Kilombero. Ndugu, Godfrey Luena ambaye aliuawa kikatili kwa kukatwa kwa mapanga na watu wasiojulikana nyumbani kwake Ifakara. Kifo cha Luena ni mwendelezo wa matukio yanayotishia maisha ya watetezi wa haki za binadamu Tanzania.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaisihi Serikali kuhalikisha hatua za kisheria zinazchukuliwa dhidi ya watakaobainika kuhusika. Luena alifanya kazi na LHRC kama mwangalizi wa haki za binadamu kwa muda mrefu na kabla ya kifo chake.



*Dkt. Helen Kijo-Bisimba (wa pili kushoto) akiwa na baadhi ya wafanyakazi wa LHRC walipofika kuhani nyumbani kwa ndugu wa Akwilina.*

# Wanahabari, Wanaharakati waahidi kukuza ushiriki wa wananchi

Wadau wa vyombo vya habari na wanaharakati wa haki za binadamu wamekutana Februari 14, 2018 katika ofisi za Makao Makuu ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kujadili namna bora ya kutatua ongezeko la ukandamizwaji wa uhuru wa kujieleza na uhuru wa kukusanyika ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika masuala ya haki za kiraia na kisiasa.

Mkutano huo umewakutanisha wawakilishi kutoka asasi mbalimbali ikiwemo Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), TWAWEZA, Mfuko wa Wanawake Tanzania, Policy Forum, WiLDAF, Umoja wa Vyama vya Siasa (TCD), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania (CHRAGG), TGNP, pamoja na wadau wa vyombo vya habari kutoka Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF. Washiriki wamekubaliana kudumisha ushirikiano katika kushawishi Serikali kufanya maboresho kisheria na kiutendaji ili kulinda uhuru wa kujieleza na uhuru wa kukusanyika kwa lengo la kudumisha ushiriki wa wananchi katika ujenzi wa taifa.

Kupitia kikao hicho, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimetambulisha mradi mpya ambao unalenga kuongeza uelewa wa wananchi juu ya sheria zinazosimamia masuala ya habari na mawasiliano sambamba na kuongeza ushiriki wa wananchi katika masuala ya kiraia na kisiasa.



*Aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) Ndugu Theophil Makunga (kulia) akifafanua jambo wakati wa mkutano wa wadau kujadili ushiriki wa wananchi katika shughuli za kimaendeleo. Mkutano huo ulifanyika Ofisi za Makao Makuu ya LHRC mnamo Februari 2018.*

# Viongozi wa Serikali watakiwa Kuheshimu Utawala wa Sheria



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaama Paul Makonda*

Katika kuhakikisha kuwa haki za binadamu na utawala wa sheria vinaheshimiwa na kulindwa nchini Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeendelea kufanya ufuatiliaji wa utendajikazi wa serikali. Kupitia utendaji kazi wa Serikali Kituo kimeona juhudi mbalimbali za kuboresha ustawi wa maisha ya wananchi ikiwemo kuwakutanisha wananchi na kusikiliza na kuweka mikakati bora ya kutatua kero zao. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua mchango wa mikutano baina ya viongozi na wananchi katika kutatua kero za wananchi na kinapongeza jitihada za viongozi mbalimbali wanaotekeleza wajibu huo.

Hata hivyo ombwe la viongozi wa serikali kutokufuata taratibu na sheria katika utekelezaji wa majukumu yao limeendelea kuathiri uhalali wa juhudi hizo. Kupitia mkutano wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndugu Paul Makonda na wananchi wa Dar es Salaam uliofanyika Februari 10, 2018, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimebaini mapungufu kadhaa ambayo yamekuwa yakifanywa si tu na Ndugu Makonda pekee bali pia na baadhi ya viongozi wengine wa serikali. Baadhi ya mapungufu ya kisheria yaliyotokana na mkutano huo ni pamoja na:

1. Kusimamisha Utendaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata Kinyume na Sheria; kwa mujibu wa Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi (2002). Mabaraza ya Ardhi ya Kata yameundwa kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi ya kata. Mabaraza hayo hupatikana kutokana na Kamati ya kata kupitia kikao cha maendeleo ya kata kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mabaraza ya Kata, 1985 Kifungu cha 4(1a). Kifungu cha 167 (1d) cha Sheria namba 4 ya Ardhi, 1999 kinayatambua mabaraza ya kata kama mahakama za ardhi kwa ngazi ya kata. Sambamba

na sheria hizo, Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro namba 216, 2002 kinayatambua mbaraza ya kata kama mahakama ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa ngazi ya kata.

Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi inamtaja Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa na mamlaka juu ya Mabaraza ya Ardhi ya Kata. Kwa mujibu wa sheria hizi Wakuu wa Mikoa hawana mamlaka ya kusimamisha, kuendesha wala kulekeza utendaji wa mabaraza ya kata katika mikoa yao. Hivyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kuwajulisha wananchi kuwa kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni batilifu na isiyokuwa na mashiko kisheria.

2. Kuingilia muhimili wa Mahakama: Ibara ya 107A – (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema "Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni Mahakama". Ibara ya 107 B inasisitiza uhuru wa mahakama katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa mujibu wa Ibara hii mihimili mingine ya dola na watendaji wake hawapaswi kwa namna yoyote ile kuingilia utendaji wa mahakama. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshuhudia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndugu Paul Makonda akishambulia utendaji wa Mahakama kinyume cha Katiba aliyoapa kuilinda. Ndugu Makonda amesikika mara kwa mara akitoa kauli za kushambulia na kukebehi utendaji wa mahakama na amerudia katika mkutano wake wa Februari 10, 2018 akisema "Mahakama haitaki kuguswa kwa kisingizio cha muhimili mwingine, wamechukua nafasi ya Mungu na mimi ni mteule wa Mungu lazima niwaseme".

Kupitia mfano huo wa ukiukwaji wa makusudi wa misingi ya utawala wa sheria Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilitoa tamko kuwakumbusha viongozi wa Serikali kuzingatia misingi ya utawala bora na utawala wa sharia.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinawakumbusha viongozi wa Serikali na wanasiasa kuwa hawana mamlaka ya kisheria kuingilia utendaji kazi wa mahakama wala kuelekeza utendaji wa Mahakama badala yake wanapaswa kuheshimu na kufuata taratibu za kimahakama katika upatikanaji wa haki. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua madhaifu yaliyopo katika vyombo vya usimamizi wa sheria na utoaji haki na kinaitaka serikali kutatua changamoto hizo ili kurahisisha upatikanaji wa haki badala ya kutumia changamoto hizo kama mtaji wa kisiasa.

# Tujenge Jamii inayopinga Ukeketaji na Kuheshimu haki za Wanawake

Tarehe 6 Februari kila mwaka ni siku ya kimataifa ya kupinga Ukeketaji duniani kote. Historia ya siku hii ilianza mwaka 2003 ambapo Baraza la Umoja wa Mataifa liliidhinisha kuwa siku rasmi ya kimataifa ya kupinga Ukeketaji duniani kote. Baraza la Umoja wa Mataifa lilifikia uamuzi huu baada ya kutathimini na kuona athari kubwa zitokanazo na vitendo vya ukeketaji kwa mtoto wa kike.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni: Pinga Ukeketaji, kwa Maendeleo ya Mwanamke na Mtoto wa Kike!

### Ukeketaji ni nini?

Ukeketaji ni kitendo cha kukata, kuvuta ama kuharibu kwa namna yoyote ile kiungo cha ndani au cha nje cha uke wa mtoto wa kike. Tendo hili hufanywa pasipokuwa na sababu zozote za kisayansi/kiafya. Ni kitendo kinachomdhalilisha mtoto wa kike na kumwondolea utu wake kama mwanandamu aliyeumbwa kamili. Historia ya utekelezaji wa mila hii potofu inasadikika kuanza yapata miaka 2000 iliyopita. Ukeketaji mara zote hufanyika kwa sababu ya misukumo ya kibinadamu, ikiwemo kupata mali kwa kumwozesha binti aliyekeketwa, kutii




*Wahanga wa ukeketaji kutoka kituo cha nyumba salama kilichopo Serengeti wakijumuika na wadau katika matembezi ya amani kupinga mila hiyo potofu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukeketaji wilayani humo.*

masharti ya mila kama ya kutambika mizimu, kuondoa mikosi katika familia, kumvusha mtoto rika na nyinginezo nyingi. Hata hivyo sababu hizo zote hazina maana zaidi ya kuendeleza tamaduni kandamizi kwa wanawake na watoto wa kike.

### Madhara ya Ukeketaji

Yapo madhara mengi yanayosababishwa na ukeketaji; madhara hayo yanaweza kuwa ya kiafya au hata kisaikolojia. Madhara yanayosababishwa na ukeketaji yanaweza kuwa ya papo kwa papo kama maumivu makali wakati wa ukeketaji, mshtuko, homa kali, kumwaga damu nyingi na mara nyingine hata kupelekea kifo, kuambukizwa magonjwa kama Virusi Vya UKIMWI na msongo wa mawazo. Yapo pia madhara ya muda mrefu kama vile; kuathirika kisaikolojia, ulemavu/kovu la kudumu katika uke, fistula, kupata shida wakati wa kujifungua na muda mwingine kupelekea kupata ugumba.

### Jitihada za wadau

Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali, Mashirika na Taasisi mbalimbali bado ukeketaji umeendelea kutekelezwa katika baadhi ya jamii. Kwa mujibu wa Takwimu za Taarifa ya Demographia na Afya ya 2012 zinaonyesha kuwa pamoja na jitihada za kutokomeza vitendo hivyo, bado kuna mikoa mitano inayoongoza kwa ukeketaji nchini ikiongozwa na Manyara wenye asilimia (58) ukifuatiwa na Dodoma (47), Arusha (41), Mara (32) na Singida yenye asilimia (31). Ziko sababu nyingi zinazosababisha, kuendelea kwa ukeketaji moja kati ya hizo ni usiri mkubwa uliopo katika jamii husika. Jamii kwa kuamini kuwa kukeketa ni mila na desturi zao, wameendelea kuhifadhi na kutunza siri za wale wanaoendeleza vitendo hivyo, ili kuwaepusha wahusika na mkono wa dola. Hali hii hupelekea watoto wa kike na wanawake kuendelea kunyanyasika bila msaada.

Mtandao wa mashirika yanayopinga ukeketaji hapa nchini umeendelea kusimama imara katika kuhahikisha kuwa ukeketaji unakoma ifikapo 2030 ili kuendana na mikakati ya maendeleo endelevu ya kidunia ya kuondoa aina zote za ubaguzi na ukatili dhidi ya wanawake na watoto na vilevile kuendana na mikakati ya kitaifa kama ilivyoainishwa katika mpango kazi wa kitaifa wa kupinga vitendo vyote vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Zipo juhudi kubwa zimefanyika katika wilaya mbalimbali nchini ikiwemo miradi ya kutoa elimu na kusaidia watoto wa kike kukabiliana na mila ya ukeketaji katika mikoa iliyotajwa. Kazi ambazo zimekuwa zikifanywa na wanamtandao ni pamoja na Mafunzo kwa wazee wa mila, ngariba, jeshi la polisi, mhimili wa mahakama, walimu, watoto, wazazi na jamii kwa ujumla ambayo yameleta chachu katika kukuza na kuimarisha uelewa wa kila mtu katika mapambano dhidi ya ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake.

Sambamba na hilo mtandao unafanya kazi kuwezesha wahanga wa ukeketaji kufikia vyombo vya kisheria ikiwemo polisi na mahakama ili kuwachukulia hatua wale wote wanaendeleza mila hii kandamizi.

Serikali imeendelea kuboresha sheria na sera mbalimbali ili kupanua wigo wa adhabu kwa wale wanaoendelea kutekeleza kitendo hicho cha kikatili. Kwa mfano mabadiliko ya Sheria ya Mtoto (2009) yamelenga pamoja na mambo mengine kupanua adhabu na kutengeneza mnyororo mpana wa washiriki. Maboresho ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu (2002) nayo yamepanua uwanda wa kutoa adhabu na kubaini kipimo cha ushiriki wa mtuhumiwa katika kufanya ukeketaji.

Sera mbalimbali za kitaifa ikiwemo Sera ya Elimu ya 2015 inapinga kila aina ya unyanyasaji kwa mtoto wa kike na inaweka na kutambua misingi ya haki na usawa kwa watoto wote wa kike na wa kiume. Sera hii pia imelenga kuondoa ubaguzi na unyanyasaji kwa mtoto wa kike.

Serikali ya Jamhuri ya Mungano pia imeendelea kuridhia na kutekeleza sera na sheria mbalimbali za kimataifa zinazolenga kutokomeza ukeketaji na unyanyasaji kwa mtoto wa kike. Tanzania imeridhia mkataba wa kimataifa wa Kupinga aina zote za Ukatili kwa wanawake CEDAW wa mwaka 1979 na mikataba mingine mingi. Kuendelea kutumika kwa sheria hizi za kimataifa na kikanda kumezidi kutanua wigo wa sheria na uwajibikaji wa kitaasisi katika kulinda masilahi ya mtoto wa kike dhidi ya ukeketaji.

Wadau wengine kama Jeshi la Polisi, Mahakama, taasisi za kidini na viongozi wa kimila wameonyesha nia na jitihada kubwa katika kuunga mkono kampeni za kutokomeza ukeketaji nchini.

## Nini kifanyike ili kutokomeza kabisa ukeketaji?

Mbali na jitihada kubwa zinazochukuliwa na wadau kutokomeza ukeketaji nchini, bado kuna mambo kadhaa ya kufanya ili kuondosha kabisa mila hii potofu katika jamii zetu.

1. Serikali kusimamia kikamilifu sheria kuhakikisha watekelezaji wa vitendo vya ukeketaji wanakamatwa na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania idumishe ushirikiano na taasisi zisizo za kiserikali pamoja na mashirika rafiki ya kimataifa ili kwa pamoja tuweze kutokomeza ukeketaji na ukandamizaji kwa mtoto wa kike na wanawake.
2. Jamii inapaswa kuungana na kukemea kwa nguvu vitendo vya ukeketaji na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ikiwemo kutoa taarifa na ushahidi ili kufanikisha vita dhidi ya ukeketaji na ukatili wa kijinsia kwa ujumla.
3. Wadau waongeze juhudi katika kuzifikia jamii zinazotekeleza mila ya ukeketaji kwa elimu na kwa msaada wa moja kwa moja ili kutokomeza janga hili.

# LHRC yapinga Ukandamizwaji wa Uhuru wa Vyombo vya Habari

Kufuatia adhabu iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa vituo vitano vya televisheni nchini ikiwemo Azam TV, ITV, Star TV, Channel 10 na EATV, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilitoa tamko Januari 3, 2018 kupinga ukandamizwaji wa uhuru wa maoni na uhuru wa kujieleza unaoendelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano nchini, vyombo hivyo vilitiwa hatiani kwa makosa matatu chini ya kifungu cha 5 na 6 vya Kanuni za Maudhui za mwaka 2005; na kupigwa faini kwa viwango tofauti pamoja na kuwekwa chini ya uangalizi kwa muda wa miezi 6.

Sambamba na kukemea ukandamizwaji huo wa uhuru wa habari kinyume na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kituo pia kilitoa salamu za pole kwa vyombo hivyo na vyombo vingine vya habari ambavyo vimekumbwa na dhoruba ya adhabu kutoka kwa serikali hasa kwa kutoa taarifa zisizoifurahisha serikali.

Kupitia hatua hiyo ya TCRA dhidi ya vyombo vya habari, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimebaini yafuatayo:

i. Kuendelea kukiuwa kwa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania, 1977 juu ya Haki ya Uhuru wa Kujieleza hususani haki kupata na kutoa taarifa juu ya masuala muhimu yanayoihusu jamii. Ibara hiyo inasema;

*"18.-(a) Kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;*
*(b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;*

ii. Vyombo vya habari kukosa uhuru wake wa kutoa taarifa kwa jamii hususani zile zinazoikosoa serikali moja kwa moja katika utekelezaji wa majukumu yake. Mathalani mwaka 2017 tumeshuhudia magazeti mbalimbali yakifungiwa na mengine kupewa onyo

iii. Serikali kupitia jeshi la polisi wamekuwa wakitumia neno "UCHOCHEZI" kuminya uhuru wa mawazo na kujieleza.

iv. Kutumika kwa mamlaka nyingine za serikali kuingilia uhuru wa kujieleza hata katika maeneo mengine ya jamii. Mathalani katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikijiingiza katika malumbano na kiongozi wa


Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship linaloongozwa na Askofu Zacharia Kakobe kwa kile tu alichokisema madhabahuni kama sehemu ya mahubiri ya ibada kanisani.

Kuongezeka kwa idadi ya viongozi wa kisiasa na wanajamii wengine kukamatwa na kuitwa kuhojiwa kwa kauli au maoni yao yasiyoipendeza serikali kinyume na misingi ya kikatiba chini ya Ibara ya 18 kama ilivyotajwa hapo juu. Mambo yote haya yanaonyesha kuwa serikali yetu haiko tayari kusikia upande unaokosoa kwa lengo la kuboresha utendaji wake. Mfano mzuri ni tamko lilitolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa vyombo vya habari Novemba 30, 2017 juu ya tathmini ya haki za binadamu katika uchaguzi mdogo wa madiwani uliofanyika mwezi Novemba 2017.

Katika tathmini hiyo Kituo kilitoa hoja kulingana na hali ilivyokuwa katika kata ambazo uchaguzi ulifanyika na kutoa mapendekezo kwa vyombo husika ili kuepusha uwezekano wa kujirudia kwa hali hiyo katika chaguzi zijazo. Tamko hilo lilijikita katika hoja na hata kutoa ushahidi wa picha, vyombo vya habari havikuwa na haja ya kufanya mizania kwenye habari ambayo imetokana na hoja (facts). Kanuni ya 8 ya Kanuni za Maudhui za mwaka 2005 inavitaka vyombo vya habari kuwa na mizania kwa taarifa za kiuchunguzi. Taarifa iliyoripotiwa na vyombo vya habari kutoka LHRC haikuwa ya kiuchunguzi hivyo haikuwa na haja ya mizania. Hata hivyo upande wowote uliohisi kuwepo kwa upotoshaji walipaswa kutumia haki yao kikatiba kutoa hoja zao na si kutumia mamlaka kuviadhibu vyombo vya habari kwa kuwasilisha hoja za LHRC.

Kufuatia ukandamizwaji huu mkubwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinawaomba watanzania kuungana kuitaka serikali kutokuchezea uhuru wa kujieleza ambao upo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# Watanzania 2577 wapatiwa msaada wa kisheria




Kupitia Kituo cha Mfano cha Msaada wa Kisheria cha Kinondoni pamoja na Kituo cha Msaada wa Kisheria Arusha na pia kupitia huduma za msaada wa kisheria wa kuhama hama LHRC imewasaidia jumla ya watanzania 2,577 (849 Wanawake na 1728 Wanaume) kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2018.

Vilevile, Kituo kimefungua vituo vinne (4) vipya vya msaada wa kisheria katika kata nne tofauti ambazo ni Somangila na Kibada katika wilaya ya Kigamboni pamoja na Mnyamani na Kitunda katika wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam.

# Habari katika Picha

**Kuwajengea Uwezo Wanafunzi**



*Ally Seif (kushoto) na Tito Magoti wakiwapa somo wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Zanaki walipotembelea Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kujifunza kuhusu haki za binadamu.*



*Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Zanaki wakiwa katika picha ya pamoja na maafisa wa LHRC Ally Seif, Richard Ng'owo na Tito Magoti walipotembelea Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kujifunza kuhusu haki za binadamu.*

**Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake**




*Wafanyakazi wa LHRC wakiongoza maandamano kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake jijini Arusha.*



*Timu ya wanasheria wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu pamoja na wanasheria wa shirika la PLPG wakiwa katika picha ya pamoja na wasaidizi wa kisheria wa Kigamboni wakati wakitoa huduma ya msaada wa kisheria kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.*



*Wanawake tunaweza! Wanawake wakionyesha ishara ya nguvu na uwezo walionao katika kufanya mambo mbalimbali wakati wa hafla ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake.*

**Mkutano na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



*Wakili Naemy Sillayo (katikati) akifafanua jambo kwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Tulia Ackson (wa kwanza kushoto) wakati wa mkutano wa utetezi dhidi ya ndoa za utotoni.*



*Wadau kutoka asasi za kiraia na vyombo vya habari wakiwa katika picha ya pamoja baada ya mkutano wa wadau kujadili ushiriki wa wananchi katika shughuli za kimaendeleo. Mkutano huo ulifanyika Ofisi za Makao Makuu ya LHRC mnamo Februari 2018.*




*Wasichana na Wanawake Wadogo wilayani Kahama wakionesha mabango yenye ujumbe kuzitaka mamlaka kuboresha huduma za afya na UKIMWI mkoani Shinyanga*

# Bodi ya Wahariri



**Dkt Helen Kijo-Bisimba**
Mkurugenzi Mtendaji



**Anna Henga**
Mkurugenzi wa Utetezi na Maboresho



**Felista Mauya**
Mkurugenzi wa Uangalizi wa Haki za Binadamu na Uwajibikaji



**Paul Mikongoti**
Asifa Programu - Dawati la Utafiti



**Naemy Sillayo**
Afisa Programu - Dawati la Jinsia na Watoto



**Fundikira Wazambi**
Afisa Programu - Dawati la Utafiti



**Michael Mallya**
Afisa Mawasiliano

# Wakati unasoma Ujumbe huu Wapo watu wanateseka kwa kushindwa kufikia huduma za haki.

Washike mkono kwa kujitolea kwa kadiri ya uwezo

## JINSI YA KUCHANGIA

airtel
vodacom
tigo

**Hatua ya 1:** Ingia kwenye menyu ya M-PESA Airtel Money au TigoPesa
**Hatua ya 2:** Chagua Lipia Bili
**Hatua ya 3:** Chagua Weka namba ya kampuni, Kisha weka 275454
**Hatua ya 4:** Ingiza namba ya kumbukumbu (1234)
**Hatua ya 5:** Weka kiasi cha Mchango
**Hatua ya 6:** Ingiza namba yako ya siri
**Hatua ya 7:** Bonyeza **OK** kutuma

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

@humanrightstz

LHRC Tanzania




## WASILIANA NASI KUPITIA

Justice Lugakingira House
Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama
S. L. P 75254, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038 / +255 22 2773048
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

## YAJAYO

1. Uzinduzi wa Ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara
2. Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari
3. Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wanachama wa LHRC
4. Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika

*Kwa Jamii Yenye Haki na Usawa*